HALMASHAURI YA MJI KONDOA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 28/04/2023 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA.**

**Waliohudhuria**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed A. Kiberenge | -D/K/Mjini | - | M/kiti |
| 2. | Mhe. Besela I. Maunga | -D/V/Maalum | - | M/M/kiti |
| 3. | Mhe. Juma I. Ng'ungu | -D/Kolo | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Zainabu H. Hemed | -D/Chemchem | - | " |
| 5. | Mhe. Abushehe I. Mbuva | -D/Kingale | - | " |
| 6. | Mhe. Issa I. Kambi | -D/Kilimani | - | " |
| 7. | Mhe. Jafari M. Ganga | -D/Suruke | - | " |
| 8. | Mhe. Rachel M. Sombida | -D/V/Maalum | - | " |
| 9. | Mhe. Kulwa S. Pazi | -D/Serya | - | " |
| 10. | Mhe. Fatuma I. Issa | -D/V/Maalum | - | " |
| 11. | Mhe. Hajat Ramla H. Abedi | -D/Bolisa | - | " |
| 12. | Ndg. Deogratius R. Nsanzugwanko | - Kny.Mkurugenzi | - | Katibu |

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Rahab Sanga | -Kaimu Mkuu Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 2. | Ndg. Shabani N. Sued | -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria |
| 3. | Ndg. Makonda Ng'oga | -Kny Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 4. | Ndg. Thecla Nyoni | -Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu |
| 5. | Ndg Simon L. Fidelis | -Kny Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari |
| 6. | Ndg. Hassan Kiseto | -Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 7. | Eng. Jeremia Longido | -Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini. |
| 8. | Ndg. Ally Mwinyikombo | -Kny Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii |
| 9. | Ndg Msafiri Mdule | -Kaimu Afisa Ardhi |
| 10. | Ndg. Hassan Mtamba | -Mkuu wa Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 11. | Ndg Thobias Mmari | -Kny Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu |



CamScanner

12. Ndg.Sekela Mwasubila -Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
13. Ndg. Alfred Chakalike -Kny.Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira.
14. Ndg. Ramadhan J. Hamis -Kny Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Mji Kondoa
15. Dkt. Emiliana Donald - Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

**KAMATI YA ULINZI NA USALAMA**

1. Ndg Andrea Ng'hwani - Katibu Tawala Wilaya
2. SSP. Yowabu Lusatila - OCD
3. Ndg. Thobiace B. Bwawa - DSO
4. SP A.A Kibwana - DPO
5. SP. Fadhiri Ngongite - O/C King'ang'a
6. ASI.Mustafa Kapingu - DIO
7. Inspector I.B. Chanyika - DFO
8. SSGT. Andrew S. Katama - M/JA(W)
9. Ndg. Musa Silungwe - DBC
10. SSGT Mboya Godgfrey - Zima moto

**MAAFISA TARAFA**

1. Ndg. Ally R. Mbena - Afisa Tarafa ya Kondoa Mjini
2. Ndg. Fred J. Bangule - Afisa Tarafa ya Kolo

**VYAMA VYA SIASA**

1. Ndg. Hija Bakari Suru - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi
2. Ndg. Ibrahimu S. Mpwapwa - Katibu wa Chama Cha Mapinduzi
3. Ndg. Adam. H. Mtopa - Katibu wa Mbunge

**WAKUU WA TAASISI**

1. Ndg. Wera Kweka - TARURA
2. Ndg. Majid Mjili - RUWASA



CamScanner

**WAANDISHI WA HABARI**

1. Ndg. Amani Imeda
2. Ndg. Elia Bakari
3. Ndg. Nizari Mafita

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Rosemary M. Mnguli
2. Ndg. Tatu N. Jabily

**MUHTA NA 22/2022/2023 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote kwenye kikao na alifungua kikao saa 6: 20 mchana baada ya kujiridhisha kutimia kwa akidi ya wajumbe.

**MUHTA NA 23/2022/2023 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa na kuridhiwa na wajumbe:

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 09/02/2022.
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Mji
5. Kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara kutoka Kamati za kudumu za Halmashauri na Kamati zisizo za kudumu.
    i. Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu
    ii. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira
    iii. Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI.
    iv. Kamati ya Fedha na Utawala.
6. Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi
7. Kufunga kikao.



CamScanner

**MUHT. NA 24/2022/2023 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 09/02/2023**

Baada ya kusomwa na kutokuwa na masahihisho yoyote muhtasari wa kikao cha tarehe 09/02/2023 ulithibitishwa na kusainiwa kuwa nyaraka halali ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

**MUHTA NA /2022/2023 MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MWENYEKITI NA MKURUGENZI**

1. **Swali kutoka kwa Mhe. Jafari Ganga wa Kata ya Suruke.**

a) Alihoji kuwa ni lini ujenzi wa ofisi za Kata utaanza kutekelezwa ili watendaji waweze kupata sehemu za kufanyika kazi.

Ufafanuzi ulitolewa kuwa suala hilo tayari limeingizwa kwenye mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2023 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Kata ili kuwajengea mazingira wezeshi watendaji wa Kata katika utekelezaji wa majukumu yao.

b) Alihoji kuhusu mipango iliyowekwa na Halmashauri juu ya kuwezesha watendaji wa Kata kuwapatia fedha kwa ajili ya kupangisha maeneo ya ofisi katika nyumba za binafsi wakati wakijiandaa katika ujenzi wa ofisi.

Ilifafanuliwa kuwa Menejimenti itasaidia kutoa fedha kwa ajili upangishaji wa maeneo ya ofisi baada ya kufanyika kwa tathmini ya kina ili kuona kama ofisi hizi zimeshindwa kujiendesha. Pia ilishauriwa watendaji wa Kata na Mitaa kuishi katika vituo vyao vya kazi tofauti na sasa ambapo walio wengi waishi nje na maeneo yao ya kazi.

2. **Swali kutoka kwa Mhe, Ramla Abedi wa Kata ya Bolisa.**

Alihoji kuhusu mpango wa uliowekwa na TARURA juu ya ujenzi wa barabara ya kutoka Mtaa wa Iboni kwenda Bolisa kwa kuwa barabara hiyo muhimu.

Ilifafanuliwa kuwa ufuatiliaji katika ngazi ya Mkoa utafanyika wakati wa kushiriki vikao vya barabara (Road Board) ili kuona kama barabara hiyo imeingizwa kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya utekelezaji na kupunguza changamoto kwa wananchi wa Kata ya Bolisa.



CamScanner

**MUHT NA 25/2022/2023 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA KUTOKA KAMATI ZA KUDUMU NA ZISIZO ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU JANUARI – MACHI, 2022/2023.**

Wenyeviti wa Kamati za kudumu na zisizo za kudumu waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na Divisheni na Vitengo zilizo chini ya Kamati zao kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2023 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika kikao cha Baraza la Waheshiwa Madiwani. Kamati zilizowasilisha taarifa ni kama ifuatavyo:-

I. **Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya aliwasilisha taarifa ya Kamati yake mbele ya wajumbe wa kikao ambapo ilielezwa kuwa Kamati ina jumla ya Divisheni na Vitengo nane ambazo ni Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Divisheni Elimu ya Awali na Msingi, Divisheni ya Elimu Sekondari, Divisheni ya viwanda, Biashara na Uwekezaji, taarifa ya Mfuko wa Bima ya Afya iliboreshwa (iCHF) na Taarifa ya Mfuko wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF). Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 14/04/2023 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2023.

Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa na kuijadili na kisha ilihojiwa kuhusu urejeshwaji wa mabati yaliyochukuliwa kutoka Shule ya Sekondari Gubali na Kwapakacha na kupelekewa kwenda kukamilisha ujenzi katika Shule Shikizi Serengeni wakati wa utekelezaji wa miradi ya UVIKO - 19. Ufafanuzi ulitolewa kuwa bati zote zilizochukuliwa zilikwisharejeshwa kwenye Shule husika.

Pia Wajumbe walihoji hatua iliyofikiwa ya utoaji wa chakula cha mchana kwa wanafunzi katika shule zote. Ufafanuzi ulitolewa kuwa jukumu hili ni la wote na sio jukumu la kamati pekee kuhakikisha kuwa chakula cha mchana kinatolewa shuleni hivyo Waheshimiwa Madiwani kupitia vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata, vikao vya wazazi ili kuhakikisha kuwa wanasimamia suala la utoaji wa chakula cha mchana shuleni ili kusaidia kupunguza utoro wa wanafunzi na kuongeza ufaulu.

Aidha, ilihojiwa idadi ya Shule Shikizi ambazo zimepangwa kusajiliwa. Ilifafanuliwa kuwa Shule Shikizi zilizokamilika na kufikia hatua ya kupata usajili ni Shule Shikizi Chang'ombe na Serengeni. Ilifafanuliwa kuwa usajili wa Shule zilizobaki utazingatia vigezo ikiwemo ukamilikaji wa vyumba



CamScanner

vya madarasa, ujenzi wa vyoo pamoja na nyumba ya mwalimu ambapo shule husika inapata sifa ya usaji na shule ambazo zimekamilika zitaandikiwa barua ya kuomba kusajiliwa.
Wajumbe walihitaji kupata ufafanuzi juu ya Mitaa ambayo wananchi wake walipatiwa elimu juu ya kilimo bora. Ilifafanuliwa kuwa elimu ilitolewa kwa mwananchi mmoja mmoja kupitia Maafisa Ugani katika maeneo yao na kwamba njia hii ya utoaji wa elimu unasaidia kutunza kumbukumbu za wakulima na kutambua idadi ya wakulima ambao wamepatiwa elimu juu ya kilimo bora katika Kata.

Ilihojiwa Kamati imeweka mikakati gani ya kuhakakikisha kuwa wanadhibiti utoro kwa wanafunzi kwa shule za Sekondari na Msingi. Ilifafanuliwa kuwa changamoto ya utoro ya wananfunzi umekuwa ukisababishwa na wazazi kwa kuwahamasisha wanafunzi kujinga na madrasa na kuacha shule, hivyo Sheria inatakiwa kutumika kuhakikisha kuwa wazazi wanachukuliwa hatua kali za kisheria ili kuwafuatilia watoto wao kwenda shule.

Wajumbe walihoji kuwa lengo la ujenzi wa vituo vya afya ni pamoja na utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi na kumpunguzia mwananchi umbali wa kwenda kufuata huduma za afya. Hivyo walihitaji kufahamu ni lini huduma za upasuaji zitaanza kutolewa katika vituo hivyo ikiwa ni pamoja na kupokelewa kwa vifaa vya kutolea huduma. Ufafanuzi ulitolewa kuwa changamoto ni uhaba wa fedha hivyo kupelelekea vifaa hivyo kutokununuliwa kwa wakati, kwasababu hiyo Halmashauri imeandika aandiko maalum kwa ajili ya kuomba kununuliwa vifaa hivyo pia imetenga fedha katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya kutolea huduma za afya kwenye vituo vya afya. Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**II. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira**

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya Kamati yake mbele ya wajumbe wa kikao ambapo alieleza kuwa Kamati hii inajumuisha Divisheni moja na Vitengo viwili ambazo ni Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini, Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira na Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira. Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 17/04/2023 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya tatu Januari - Machi, 2023.



CamScanner

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kisha ilielezwa kuwa hali ya usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Mji bado hairidhishi kwa sasababu maeneo mengi ni machafu kutokana na utupaji hovyo wa taka katika Mitaa.

Pia ilielezwa kuwa sababu nyingine inayochangia uchafu katika Mji ni ucheleweshaji wa urejeshaji wa fedha za uzoaji taka na ukosefu wa gari maalum kwa ajili ya kubeba taka taka. Halmashauri ina gari moja ambalo pia linatumika katika usambazaji wa matofali kwenye miradi inayoendelea kutekelezwa na hivyo kushindwa kuzoa taka kwa wakati.

Hivyo kamati inashauri Menejimenti kurejesha fedha kwa wakati katika mitaa ili zitumike katika kukodi magari kwa wakati kwa ajili ya kuzoa taka. Pia ilishauriwa Waheshimiwa madiwani kuhamasisha ufanyikaji wa usafi katika Mitaa yao pamoja na watendaji Mitaa na Kata kusimamia kamati za mazingira ili zitekeleze jukumu la kuhakikisha usafi wa mazingira unafanyika.

Wajumbe walishauri kuwa mchakato wa ubinafsishaji wa chanzo cha mapato ya usafi wa mazingira ukamilike ili kuimarisha usafi wa mazingira katika Mitaa yote ya Halmashauri ya Mji na kuongeza mapato.

Pia ilielekezwa kuwa Halmashauri itashirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuendelea kusimamia utunzaji wa mazingira katika maeneo yote ya Halmashauri ya Mji.

Aidha, Ilishauriwa kutumika kwa Sheria ndogo za Halmashauri ya Mji kwa ajili ya kuwachukulia hatua wananchi wanaokata miti hovyo na kulima katika maeneo ya hifadhi ya milima.

Vilevile, wajumbe walihoji ni lini upimaji uliofanyika katika eneo la Mtaa wa Maji ya Shamba utakamilishwa ili wnanchi wa eneo hilo waweze kupatiwa hati za umiliki wa maeneo yao. Ilifafanuliwa kuwa Menejimenti itafanya ufuatiliaji wa suala hilo.

Taarifa ya Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

### III. Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya VVU na UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU aliwasilisha taarifa ya utakelezaji wa shughuli za Kamati mbele ya wajumbe wa kikao, ambapo alieleza kuwa Kamati hiyo inajumuisha Divisheni mbili ambazo ni Divisheni ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe na Divisheni ya Maendeleo ya Jamii. Alieleza kuwa Kamati ilifany kikao tarehe 18/04/2023 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2022/2023.



CamScanner

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU ilipokelewa na kuiridhiwa na wajumbe.

### IV. Kamati ya Fedha na Utawala

Kwaniaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Utawala Mhe. Diwani ambaye ni mjumbe wa Kamati aliwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya wajumbe ambapo alieleza kuwa Kamati inajumuisha Divisheni na Vitengo sita ambazo ni Divisheni ya Mipango na Uratibu, Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Huduma za Sheria, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Kitengo cha Fedha na Uhasibu na Kitengo cha TEHAMA na Takwimu. Alieleza kuwa Kamati ilifanya vikao vyake tarehe 28/02/2022, 23/03/2022 na 24/04/2023 na kujadili na kupitisha masuala mbalimbali pamoja na taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na Divisheni na Vitengo kwa kipindi cha robo ya tatu Januari - Machi, 2023. Taarifa ya mapato na matumizi pamoja na fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ziliwasilishwa kama ifuatavyo:-

#### a) Mapato na matumizi

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Mji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 iliidhinishiwa kukusanya jumla ya Shilingi 19,912,978,000.00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Ilifafanuliwa kuwa Halmashauri ilivuka mwaka na bakaa ya kiasi cha Shilingi 785,078,798.00 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hivyo kupelekea bajeti ya utekelezaji kuwa kiasi cha shilingi 20,698,056,798.00

Aidha, katika kipindi cha mwezi Machi, 2023 Halmashauri ilikusanya kiasi cha Shilingi 1,037,128,982.59 ambayo ni sawa na asilimia 61 ya makusanyo ya mapato ya mwezi na kufanya jumla ya makusanyo yote ya kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi mwezi Machi, 2023 kuwa kiasi cha shilingi 12,237,084,398.98 ya mapato yote kwa mwaka 2022/2023. Mapato hayo kwa kipindi cha Machi, 2023 yaliainishwa kama ifuatavyo; -

| | | |
|---|---|---|
| i. Vyanzo vya mapato ya ndani halisi | - | 57,076,955.05 |
| ii. Mapato ya kisekta | - | 31,175,931.54 |
| iii. Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) | - | 40,308,000.00 |
| iv. Ruzuku ya Mishahara | - | 832,745,000.00 |



CamScanner

v. Miradi ya Maendeleo - 75,823,096.00

Pia ilielezwa kuwa Halmashauri ilidhinishwa kutumia jumla ya kiasi cha Shilingi 19,912,978,000.00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikijumuishwa na bakaa ya mwaka wa fedha 2021/2022 ya kiasi cha shilingi 785,078,798.00 na kufanya jumla ya makisio ya matumizi ya fedha zote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwa kiasi cha shilingi 20,698,056,798.00.

Aidha, ilifafanuliwa kuwa katika kipindi cha mwezi Machi, 2023 Halmashauri ilitumia kiasi cha Shilingi 1,064,887,692.35 na kufikisha jumla ya matumizi yote kuwa kiasi cha shilingi 11,387,003,300.00 sawa na asilimia 57 ya makisio ya matumizi ya fedha zote kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Matumizi hayo kwa kipindi cha mwezi Machi, 2023 yaliainishwa kama ifuatavyo; -

i. Mapato ya ndani halisi - 40,373,690.00

ii. Mapato ya Kisekta - 54,614,061.00

iii. Ruzuku ya Serikali Kuu (OC) - 50,263,277.00

iv. Ruzuku ya Serikali Kuu Mishahara - 832,975,000.00

v. Miradi ya Maendeleo - 955,985,668.02

**b). Miradi ya maendeleao**

Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kwa kipindi cha robo ya tatu Januari – Machi, 2023 kama ifutavyo:-

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023, Halmashauri iliidhinishiwa shilingi. 6,252,135,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao-;

**Jedwali Na.1** Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa, zilizopokelewa na zilizotumika

| Na | Chanzo cha Fedha | Fedha idhinishwa kwa mwaka 2022/23 | Fedha pokelewa hadi Machi, 2023 | Fedha tumika hadi Machi, 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ELIMU BILA MALIPO | 758,930,000.99 | 545,168,738.76 | 545,168,738.76 |
| 2 | MITIHANI | 400,816,000.00 | 368,360,000.00 | 368,360,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | SERIKALI KUU | 1,834,250,000.00 | 1,834,250,000.00 | 969,106,700.00 |
| 4 | MFUKO WA JIMBO | 50,386,000.00 | 50,386,000.00 | |
| 5 | GLOBAL FUND | 14,169,000.00 | 2,450,000.00 | 2,450,000.00 |
| 6 | TASAF | 1,052,819,000.00 | 514,746,865.00 | 514,746,865.00 |
| 7 | HEALTH BUSKET FUND | 107,918,000.00 | 59,470,900.00 | 59,470,900.00 |
| 8 | S/KUU (NJE YA BAJETI) | | 180,000,000.00 | 180,000,000.00 |
| 9 | UNICEF (POLIO) | | 23,160,500.00 | 23,160,500.00 |
| 10 | EP4R | | 250,000,000.00 | 244,848,000.00 |
| 11 | NTD | | 8,704,494.00 | 8,704,494.00 |
| 12 | GPE LANES | | 55,824,000.00 | 0.00 |
| 13 | GLOBAL FUND (WODI) | | 25,005,895.00 | 25,005,895.00 |
| 14 | UNICEF (VYETI) | 10,000,000.00 | - | - |
| 15 | GAVI (CHANJO) | 45,471,000.00 | - | - |
| 16 | SEQUIP | 573,000,000.00 | - | - |
| 17 | EGPAF | 57,810,000.00 | - | - |
| 18 | LISHE | 56,566,000.00 | - | - |
| 19 | BOOST | 1,290,000,000.00 | - | - |
| 20 | **Jumla** | **6,252,135,000.00** | **3,917,527,392.76** | **2,941,022,092.76** |

**Mapato ya fedha za miradi**

Hadi kufikia mwezi Machi, 2023, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha shilingi. 3,917,527,392.76 kutoka katika vyanzo mbalimbali Shilingi 2,978,164,738.76 kutoka Serikali Kuu na Shilingi 939,362,654.00 kutoka kwa wahisani. Aidha kiasi cha shilingi 542,694,889.00 kimepokelewa nje ya Bajeti.

Ilifafanuliwa kuwa katika kipindi cha robo ya tatu Januari hadi Machi, 2022/23 Halmashauri ya Mji Kondoa ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 744,564,303.00 kutoka vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo;-

a. ELIMU BILA MALIPO Shilingi 180,569,403.00
b. UNICEF – POLIO shilingi 170,000.00,
c. TASAF 68,530,000.00,

d. BUSKET FUND 59,470,900.00,

e. GPE LANES 55,824,000.00

f. SERIKALI KUU 380,000,000.00.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**TAARIFA KUTOKA KWA TAASISI ZA SERIKALI TARURA, RUWASA NA TANESCO.**

Katika kikao cha Baraza la Waheshimiwa Madiwani robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 taasisi zilizopo katika Halmashauri ya Mji Kondoa zilialikwa kwa ajili ya kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na taasisi husika kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Januari hadi Machi, 2023 ambazo ni TARURA na RUWASA.

Wajumbe walihoji maswali mbalimbali ambayo yaliweza kupatiwa majibu ya kina na ushauri mbalimbali ulitolewa kwa Taasisi hizo unaotakiwa kuzingatiwa wakati wa utekelezaji miradi katika maeneo ya Halmshauri ya Mji Kondoa.

**MUHT NA 26/2022/2023TAARIFA MBALIMBALI KUTOKA KWA MKURUGENZI NA MHE. MWENYEKITI.**

Mwenyekiti alisisitizwa yafuatayo kuafanyiwa kazi;-

i. Kufanyika kwa msawazo wa walimu katika Shule za Msingi na Sekondari kwa kuzingatia wingi wa wanafunzi na mahitaji kwa kila Shule.

**NASAHA KUTOKA KWA MWENYEKITI WA CHAMA CHA MAPINDUZI**

Alitoa pongezi kwa Waheshimiwa Madiwani kwa uendeshaji mzuri wa vikao na alisisitiza kuzingatiwa kwa kanuni za uendeshaji wa vikao kwa Wakuu wa Divisheni na Vitengo kushiriki na kuwa watulivu wakati kikao kikiendelea.

Aidha, alisisitiza kuwa fedha zinazopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi zitumike kwa wakati. Pia ilishauri Wakuu wa Divisheni na Vitengo kuwashirikisha viongozi waliopo katika kamati za miradi pamoja na kuwajengea uelewa wa kutosha katika usimamizi wa miradi wanayotekelza.

Waheshimiwa Madiwani walisistizwa kuwaeleze wananchi mafanikio yote yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya sita ili kwatambue juhudi na kazi zinzofanywa na serikali yao inayoongozwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.



CamScanner

**NASAHA KUTOKA TAKUKURU**

Kamanda wa TAKUKURU Wilaya ya Kondoa alitambulisha mradi mpya unaojulikana kama TAKUKURU rafiki ambao unalenga kuimarisha masuala ya utawala bora. Pia ilielezwa kuwa kero zote za wananchi zitatatuliwa katika ngazi za kata na mchakato mzima wa utatuzi utafuatiliwa na ngazi ya TAKUKURU Wilaya ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi.

**MUHT NA 27/2022/2023KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti kabla ya aliwashukuru wajumbe wote kwa mawazo yenye tija na iliagiza Menejimenti kufanya utafiti ili kubainisha sababu zilizopelekea kushuka kwa ufaulu katika matokeo ya mitihani ya Kitaifa iliyofanyika mwaka 2022 kwa baadhi ya Shule za Sekondari na kupendekeza nini kifanyike ili kuinua ufaulu katika Shule hizo. Pia alisisitiza Kamati za mazingira kusimamia usafi wa mazingira pamoja na watumishi wa afya kutoa huduma kwa weledi kwa wananchi. Aidha, alishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuimarisha suala zima la ulinzi na usalama. Aliwatakia safari njema warejeapo majumbani mwao alifunga kikao saa 10 : 30 jioni.

**Umethibitishwa**

..............................

Jina M. M. SWEYA

**Katibu**

..............................

Jina MOHAMED KIBERENGE

**Mwenyekiti**

1/08/2023

**Tarehe.**



CamScanner